

**Changamoto Kwa Watu Wa  
Mungu – Wakristo**  
**(A Challenge To The Lord's People  
– Christians)**

**Na**

**John Kombo**

# **Changamoto Kwa Watu Wa Mungu – Wakristo**

**Na**

**John Kombo**

**Augusta 20, 2014**

# Changamoto Kwa Watu Wa Mungu – Wakristo

Nimewekeza kwa zaidi ya miaka ishirini na moja ya maisha yangu nikihubiri na kufundisha neno la Mungu (injili ya Yesu Kristo) kwa watu wengi Kenya. Ndugu Ellis alituambia kwamba ametumia zaidi ya miaka hamsini na nne akihubiri Marekani na sehemu zingine duniani. Lakini bado kuna changamoto kwa wengi wetu wanao kiri kuwa Wakristo. Je! Tunatambua kuwa Shetani anaendelea kuwa kazini? Malengo yake ni kuangamiza kila nafsi ambayo haipo tayari kujikinga yenyewe katika maisha haya au hata kupambana na kifo

Sikiliza! Kwenda katika ibada kila juma pili haitoshi kumfanya mtu awe mwaminifu kwa Bwana. Kuwa “mwema” kwa ukarimu haitoshi kumfanya mtu ahesabiwe kuwa ni kwaminifu. Bwana wetu Yesu Kristo alisema, “*Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda ataliondoa; na kila tawi lizaalo matunda atalitunza ilikwamba liveze kuzaa matunda zaidi.*” (Yoh. 15:2). Wengine wetu tumejaliwa kusikia na kujifunza kuhusu injili ya Yesu Kristo kwa watu wema kama ndugu Ellis katika maisha yetu, lakini je tuna fanya nini na hiyo injili? Mwingine anaweza kutumia ujuzi alioukata kutengeneza maisha, atapata uzuri gani? Wakristo wengi waliofundishwa hawatumii injili na kuwasaidia wengine kufanyika na kukua katika Kristo. Wakristo wa kweli, kulingana na maandiko, ni wanajeshi waliofundishwa kukabiliana na magumu, mateso, hata tishio la kifo (Warumi 8:35-36; Ufunuo 2:10).

Hebu sisi sote tuzinduke katika changamoto; wazee, mashemasi, wahubiri, walimu, wakubwa, wadogo, washirika wote wa kanisa la Bwana kila mahali.

Wale walio na nafasi kufundisha hebu na tufundishe na kuwavuvia wengine kuwa watendaji katika kazi ya Bwana.

Tuwafundishe watoto wetu na vijana kwamba Biblia ndio mwongozo wao katika maisha. Siyo kitabu cha hadithi wala cha maneno ya kale. Wainjilist, hebu na tuingie katika jamii wanaotuzunguka na kuwafundisha waliopotea. Tuisubiri hadi waje. Hawatakuja.

Mwisho, ndugu na dada, unafanya nini, binafsi kama Mkristo? angalia nafasi yoyote ya kuleta vitu vya kiroho katika mazungumzo na marafiki na ndugu zako. Boresha uhusiano, kwa malengo ya kushiriki injili na mtu huyo, ukiwaombea kwa dhati.

“*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu kwa hekima yote, mkifundishana na kuonyana ninyi kwa ninyi...*” (Wakolosai 3:16).

John Kombo Nandwa  
Nakuru, Kenya







